

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BARAZA LA MITIHANI
UPIMAJI WA ELIMU YA MSINGI DARASA LA PILI

201 STADI YA KUSOMA

Muda: Dakika 15 Jumanne, 24 Novemba 2015 asubuhi

Maelekezo

1. *Karatasi hii ina maswali matatu.*
2. *Mwanafunzi anatakiwa kujibu maswali yote kwa kusoma.*
3. *Kila mwanafunzi atapimwa kwa dakika 15.*
4. *Msimamizi anatakiwa kujaza taarifa za mwanafunzi katika nafasi zilizo wazi kwenye kona ya juu ya kulia mwa karatasi ya skeli ya upimaji kwa kalamu ya wino wa bluu.*
5. *Mwanafunzi atakapokuwa amemaliza kusoma, msimamizi anatakiwa kujaza alama katika karatasi maalum ya skeli ya upimaji aliyopewakwa kutumia kalamu ya wino mwekundu.*

Kusoma Maneno

Mwongoze mwanafunzi kusoma maneno kwa kuzingatia yafuatayo:

- (a) Mwoneshe mwanafunzi (kwa kugusa kwa kalamu) kuanzia neno la kwanza kutoka kushoto kwenda kulia katika kila mstari.
- (b) Mwelekeze mwanafunzi kusoma maneno kwa sauti, umakini na haraka kadri awezavyo.
- (c) Hakikisha kuwa mwanafunzi anatumia **sekunde tatu** tu kusoma neno. Baada ya sekunde tatu mwelekeze mwanafunzi kusoma neno linalofuata.
- (d) Usomaji wa maneno yote utafanyika kwa **dakika tatu**, ambapo **dakika moja** itatumiwa na mwanafunzi katika usomaji na **dakika mbili** zitatumiwa na msimamizi katika ukokotoaji wa alama na ujazaji wakaratasi ya skeli ya upimaji.

1. Mwanafunzi asome maneno yafuatayo:

<i>Jua</i>	<i>asubuhi</i>	<i>tano</i>	<i>simba</i>	<i>mchezo</i>
<i>wazazi</i>	<i>chungwa</i>	<i>shati</i>	<i>watu</i>	<i>weka</i>
<i>kimbia</i>	<i>panya</i>	<i>vitabu</i>	<i>siku</i>	<i>kijani</i>
<i>tisa</i>	<i>rubani</i>	<i>maji</i>	<i>asante</i>	<i>mguu</i>

Kusoma Sentensi

Mwongoze mwanafunzi kusoma sentensi kwa kuzingatia yafuatayo:

- (a) Mwoneshe mwanafunzi (kwa kugusa kwa kalamu) kuanzia sentensi ya kwanza kutoka kushoto kwenda kulia katika kila mstari.
- (b) Mwelekeze mwanafunzi kusoma sentensi kwa sauti, umakini na haraka kadri awezavyo.
- (c) Hakikisha kuwa mwanafunzi anatumia **sekunde tatu** tu kusoma neno. Baada ya sekunde tatu mwelekeze mwanafunzi kusoma neno linalofuata.
- (d) Usomaji wa sentensi zote utafanyika kwa **dakika nne**, ambapo **dakika moja** itatumiwa na mwanafunzi katika usomaji na **dakika tatu** zitatumiwa na msimamizi katika ukokotoaji wa alama na ujazaji wa karatasi ya skeli ya upimaji.

2. Mwanafunzi asome sentensi zifuatazo:

Magari ni mazuri sana.

Wazazi wangu ni wakarimu.

Mwalimu wetu ni mzuri.

Mimi nilifua nguo zangu.

Tanzania ni nchi yangu.

Kusoma Kifungu cha Maneno

Mwongoze mwanafunzi kusoma kifungu cha maneno kwa kuzingatia yafuatayo:

- (a) Mwoneshe mwanafunzi kifungu cha maneno (kwa kugusa kwa kalamu) kuanzia sentensi ya kwanza kutoka kushoto kwenda kulia katika kila mstari na mweleze mwanafunzi kuwa akimaliza kusoma, utachukua karatasi na utamuuliza maswali yanayohusiana na habari aliyoisoma.*
- (b) Mwelekeze mwanafunzi kusoma kifungu cha maneno kwa sauti, umakini na haraka kadri awezavyo. Mwanafunzi atakapokuwa anasoma, fuatilia usomaji wake kwa kutumia kifungu cha maneno kilichopo katika Skeli ya Upimaji.*
- (c) Mwanafunzi akimaliza kusoma chukua karatasi yake kisha muulize maswali yaliyopo katika **karatasi maalum** ya skeli ya upimaji uliyopewa.*
- (d) Usomaji wa kifungu cha maneno utafanyika kwa **dakika nane**, ambapo dakika **tatu** zitatumwa na mwanafunzi katika usomaji na dakika **tano** zitatumwa na msimamizi katika kuuliza maswali kwa mdomo, ukokotoaji wa alama na ujazaji wa karatasi ya skeli ya upimaji.*

3. *Mwanafunzi asome kifungu cha maneno kifuatacho kisha ajibu maswali atakayoulizwa kwa mdomo:*

Baraka na Tumaini ni marafiki, wanaishi kijiji cha Mtakuja. Watoto hawa

wanasoma katika shule ya msingi Mtakuja.

Wote wako darasa la pili. Walimu wao wanawapendasana,

kwa sababu wana akili. Katika matokeo ya muhulauliopita,

Tumaini alikuwa wa kwanza. Rafiki yake

alikuwa wa pili darasani kwao. Wote

wawili walifurahi sana. Katika sherehe

ya kufunga shule, wote wawili waliopewa zawadi
